# PDPC FARAGHA NEWSLETTER

ISSN 0000-0000 Na. 0003

JULAI-SEPTEMBA 2025



# KAMPENI ZIZINGATIE ULINZI WA FARAGHA KWENYE TAARIFA BINAFSI ZA WATU

Mkurugenzi Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Ofisi ya Zanzibar, **Bi. Rehema Abdalla** amewataka wagombea wa ngazi zote nchini kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 kuhakikisha hawaingilii faragha za watu. >> **UK.7**

## Elimu ya Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi yawafikia Wanawake Wahasibu Nchini.

Wakili Humphrey Mtuy, Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) ameshiriki mkutano wa nane (8) wa Uongozi wa Wanawake - 2025 ulioandaliwa na Chama cha Wahasibu wanawake Tanzania Tanzania (TAWCA) na kufanyika Jijini Arusha kuanzia Septemba 17, 2025 hadi Septemba 19, 2025. UK. 12

## Kusafirisha Taarifa Binafsi Nje ya Nchi ni lazima uwe na Kibali cha PDPC.

"Hata wale wanaosafirisha taarifa binafsi kwa ajili ya kwenda kuzitunza mtandaoni **'Cloud Server'** wanapaswa kupewa kibali na PDPC na wakati wa kuomba kibali hicho wanatakiwa kusema hiyo **'server'** ipo nchi gani, mtoa huduma ni nani na ni taarifa zipi wanazozisafirisha**" Amesema Bw.Mungy**

**Nikosa kusambaza Taarifa za mtu kwenye mitandao ya kijamii bila ridhaa yake** >> **UK.8**

**MAKALA MAALUMU:**

**Vyeti vya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) na Faida zake kwa Taasisi za Kibiashara Nchini.** >> **UK.10**

# YALIYOMO

07. Kampeni zizingatie Ulinzi wa Faragha kwenye Taarifa Binafsi za watu.

08. Nikosa kusambaza Taarifa za mtu kwenye mitandao ya kijamii bila ridhaa yake.

09. Kusafirisha Taarifa Binafsi Nje ya Nchi ni lazima uwe na Kibali cha PDPC.

10. MAKALA MAALUMU:
Vyeti vya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) na Faida zake kwa Taasisi za Kibiashara Nchini.

12. Elimu ya Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi yawafikia Wanawake Wahasibu Nchini.



# BODI YA WAHARIRI



**Mwenyekiti**
**Dkt. Emmanuel Mkilia**



**Mjumbe**
**Mhandisi Stephen Wangwe**



**Mjumbe**
**Wakili Humphrey Mtuy**



**Mjumbe**
**Dkt. Noe Nnko**



**Mjumbe**
**Rehema Abdallah**



**Mhariri Mkuu**
**Innocent Mungy**



# SALAMU KUTOKA KWA MKURUGENZI MKUU

**Ndugu Msomaji,**
Kwa niaba ya uongozi na watumishi wote wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) napenda kukukaribisha kwenye toleo hili la jarida letu la ofisi kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2025.

Jarida hili limeandaliwa kwa dhumuni la kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kulinda taarifa binafsi pamoja na kueleza hatua tulizochukua katika kutekeleza majukumu yetu ya kisheria katika kipindi hiki.

Mambo Muhimu Katika Toleo hili

- **Utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi**
- **Uhamasishaji na utoaji wa elimu kwa wadau**
- **Utoaji wa elimu kwa wadau kuimarisha uzingatiaji wa sheria na kanuni za ulinzi wa taarifa binafsi**

Tume imeendelea kuimarisha mifumo, kufanya tathmini, na kuweka utaratibu madhubuti wa kuhakikisha taarifa binafsi zinahifadhiwa na kutumiwa kwa mujibu wa Sheria. Natumaini kuwa jarida hili litakupatia maarifa sahihi, kukupa mwanga juu ya kazi zetu, na kuwa chachu ya kuongeza ushirikiano kati ya Tume na wadau wote.

Asante na karibu sana kusoma toleo hili.
**Dkt. Emmanuel L. Mkilia**
**Mkurugenzi Mkuu - PDPC**

## PDPC KUANZISHA ITHIBATI KWA MAAFISA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI (DPOs) NCHINI

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) ipo katika mpango wa kuwa na Ithibati kwa Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPOs) ili kuhakikisha ulinzi wa taarifa binafsi nchini unazingatiwa.

Hatua hii inalenga kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi na kuhakikisha kuwa waliopewa jukumu la ulinzi wa faragha za taarifa hizo wanazingatia viwango vya juu vya ufanisi na uadilifu.

Hayo yalisemwa tarehe 16/07/2025 na Mkurugenzi Mkuu wa PDPC Dkt. Emmanuel Mkilia alipotembelea kituo cha mafunzo maalum ya maafisa ulinzi wa taarifa kilichopo kwenye hoteli ya Morena, Morogoro na kuzungumza na washiriki wa mafunzo hayo ambapo alisisitiza kuwa mafunzo hayo ni hatua muhimu ya kuleta mazingira rafiki na yenye ufanisi kati ya PDPC na DPOs.




**Mkurugenzi Mkuu wa PDPC, Dkt. Emmanuel Mkilia** akizungumza na Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPOs) wakati wa Mafunzo Maalumu ya DPOs yaliyofanyika Morena Hotel Morogoro, Julai 16, 2025.

"Tunatarajia kuanzisha mfumo wa mafunzo utakaoakisi uthibitisho wa kitaalamu wa DPOs. Hii inamaanisha kwamba, bila cheti rasmi cha utambuzi wako kutoka PDPC, huwezi kuwa DPO halali," alisisitiza Dkt. Mkilia.

Hii ni hatua madhubuti inayolenga kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi, kuhakikisha maafisa wanaotekeleza majukumu haya wanazingatia viwango vya kitaifa na kimataifa, na kuleta ufanisi wa kiutendaji katika sekta hiyo muhimu kwa ulinzi wa faragha kwenye taarifa binafsi za watu na mashirika nchini.

## WAANDISHI WA HABARI NA MAAFISA HABARI WANAJUKUMU MUHIMU LA KULINDA FARAGHA ZA WATU

Katika kuhimiza usalama wa taarifa binafsi na kulinda haki za watu, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia, amezungumza na waandishi wa habari na maafisa habari wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu jukumu lao muhimu katika kulinda faragha na taarifa binafsi za wananchi.

Akizungumza Julai 19, 2025 katika mafunzo maalum yaliyofanyika ukumbi wa BOT Kinazini, Zanzibar, Dkt. Mkilia alisisitiza kuwa waandishi wa habari ni nguzo muhimu katika kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kulinda taarifa binafsi dhidi ya matumizi mabaya na uvunjifu wa sheria.

"Katika zama hizi za ukuaji wa Iteknolojia ya hali ya juu, taarifa zinaenea kwa kasi kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vingine vya habari, hivyo ni muhimu kwa waandishi wa habari kujua mbinu za kuhifadhi na kusambaza taarifa kwa ufanisi na usalama," alisema Dkt. Mkilia

Aliongeza kuwa, waandishi na maafisa habari wanapaswa kuwa na uelewa wa kina kuhusu sheria zinazohusu faragha na ulinzi wa taarifa binafsi na kutumia mbinu bora za uhariri wa taarifa ili kuepusha makosa yanayoweza kusababisha uvunjifu wa haki za watu.

Aidha, aliwataka waandishi kuzingatia kujiridhisha na vyanzo vya habari na kutumia mifumo salama ya kuhifadhi taarifa.

Mafunzo haya yanalenga kuwajengea uwezo waandishi wa habari na maafisa habari wa serikali ili wawe sehemu ya juhudi za kitaifa za kulinda faragha za wananchi, huku wakizingatia haki, sheria, na teknolojia mpya zinazoongezeka kwa kasi.

Kwa mujibu wa Dkt. Mkilia, juhudi hizi ni muhimu katika kuhakikisha taarifa binafsi zinatunzwa kwa umakini, na kwamba uhusiano kati ya vyombo vya habari na ulinzi wa taarifa ni nguzo muhimu katika kulinda haki za binadamu na ustawi wa jamii kwa ujumla.

# TAHARIRI YA MHARIRI



Karibu kwenye Jarida la Faragha.
Jarida hili limelenga kukuletea taarifa mbalimbali za shughuli zinazotekelezwa na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) ili kukujengea uelewa juu ya dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Kwa wakati tuliopo, dunia ya kidijitali imebadilisha namna tunavyokusanya, kuhifadhi na kutumia taarifa. Kadiri teknolojia inavyokua, ndivyo umuhimu wa kulinda taarifa binafsi unavyozidi kuwa mkubwa. Kwa muda mrefu, taarifa binafsi za watu zimekuwa zikisambazwa, kuhifadhiwa au kutumika bila uangalizi wa kutosha. Hali hii imeweka hatarini haki ya faragha ya kila raia.

Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi imeweka msingi thabiti wa kuhakikisha kwamba taasisi za umma na binafsi zinaheshimu na kulinda taarifa wanazokusanya. Hata hivyo, utekelezaji wake unahitaji zaidi ya maneno, yaani unahitaji mabadiliko ya fikra, mienendo, na mifumo ya namna utekelezaji wa shughuli katika maeneo yetu ya kazi. Ni lazima kila taasisi ijipange kuhakikisha watumishi wake wanaelewa wajibu wao wa kulinda taarifa za wananchi, na kuweka mifumo salama ya kuhifadhi taarifa hizo.

Tume inatoa wito kwa viongozi wote, watumishi wa umma, na wadau wa sekta binafsi kuacha kufanya ulinzi wa taarifa kuwa jambo la hiari badala yake, tuchukulie kama jukumu la kisheria, kimaadili na kitaifa. Kulinda taarifa binafsi ni kulinda utu, heshima na usalama wa kila raia.

Wakati wa kubadilika ni sasa tusisubiri tukumbushwe, bali tuwe mstari wa mbele katika utekelezaji wa matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 (PDPA) kwa vitendo.

Joseline Chambasi
**Kaimu Mhariri Mkuu**





Mkurugenzi Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Ofisi ya Zanzibar, **Bi. Rehema Abdalla** akizungumza na Mtangazaji wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) Bi. Nasra Khatib ambae hayupo pichani.

# KAMPENI ZIZINGATIE ULINZI WA FARAGHA KWENYE TAARIFA BINAFSI ZA WATU

Mkurugenzi Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Ofisi ya Zanzibar, **Bi. Rehema Abdalla** amewataka wagombea wa ngazi zote nchini kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 kuhakikisha hawaingilii faragha za watu.

Bi. Rehema amezungumza hayo wakati akifanya mahojiano maalum na mtangazaji wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) Bi. Nasra Khatib kuhusu umuhimu wa kulinda taarifa binafsi katika kampeni za uchaguzi mkuu kwa wagombea watakaonadi sera za vyama vyao.

"Wagombea wa ngazi zote hakikisheni hamuingilii faragha za watu na majukwaa mnayotumia kunadi sera za vyama vyenu yasitumike kukiuka misingi ya Sheria ya Ulinzi wa taarifa binafsi" amesema Bi. Rehema.

Akisisitiza swala hili, Bi. Rehema amesema kuwakuchapisha taarifa binafsi za mtu kwenye magazeti, mitandao ya kijamii au kutangaza kwenye redio na televisheni bila ridhaa ya muhusika wa taarifa hizo ni kinyume na matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44.

Elimu juu ya dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa makundi mbalimbali ya kijamii ni endelevu na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi inatoa elimu hiyo kuwajengea uelewa wahusika wa taarifa binafsi na watumiaji wa taarifa hizo ili uzingatiaji wa ulinzi wa faragha upewe kipaumbele wakati wa kutumia taarifa husika.





## NI KOSA KUSAMBAZA TAARIFA ZA MTU KWENYE MITANDAO YA KIJAMII BILA RIDHAA YAKE

Jamii yakumbushwa kutokusambaza au kutumia taarifa za mtu bila ridhaa ya mwenye taarifa.

Ushauri huo wa kisheria ulitolewa Agosti 20, 2025 na Wakili Godfrey Assenga, Mwanasheria wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) wakati akijibu swali la mmoja wa washiriki wa Mafunzo Maalumu ya Maafisa Ulinzi wa Taarifa (DPO's) yaliyofanyika Morena Hoteli Mkoani Morogoro, ambapo aliulizwa je wale wanaosamba taarifa za watu kwenye makundi sogozi (WhatsApp groups) bila kuwa na ridhaa ya wahusika wa taarifa hizo nao wanavunja Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 (PDPA)?

Akijibu swali hilo Wakili Asenga alisema, ndio ni kosa kisheria kwa mujibu wa Kanuni za Ukusanyaji na Uchakataji wa Taarifa Binafsi za mwaka 2023 na akasisitiza hata wale wanaosamba taarifa za watu kupitia mitandao ya kijamii hawaruhusiwi kufanya hivyo kama hawajapata ridhaa ya muhusika wa taarifa.

"Kanuni ya 15 (1) ya Kanuni za ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi za mwaka 2023 inasema muhusika wa taarifa anaweza kuomba kwa mkusanyaji au mchakataji kusitisha mara moja ukusanyaji au uchakataji wa taarifa zake binafsi muda wowote, hivyo muhusika wa taarifa akiomba ridhaa ya kufutwa kwa taarifa zake unapaswa kumsikiliza na kuzifuta na endapo ukikaidi ombi lake ana haki ya kuja kulalamika PDPC na Sheria itafata mkondo wake" Alisema Wakili Assenga

Aidha Wakili Assenga alihitimisha kujibu swali hilo kwa kunukuu msemo maarufu wa kutokujua Sheria sio kigezo cha kuvunja Sheria.



## JENGA UAMINIFU WA TAASISI YAKO KWA WADAU KWA KULINDA TAARIFA ZAO BINAFSI.

Ikiwa ni siku ya kwanza ya awamu ya nne ya mafunzo maalum kwa Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPO) kutoka kwenye taasisi za umma na binafsi nchini, maafisa hao wametakiwa kuhakikisha taarifa binafsi za wadau wa taasisi zao zinalindwa kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44.

Akitoa mafunzo hayo Bi. Hellen Achimpota tarehe 20 Agosti, 2025 mkoani Morogoro amesema ni muhimu kuzingatia ukusanyaji wa taarifa binafsi unafanywa kwa lengo maalum tu, na kuhakikisha kuwa taarifa hizo hazitumiki nje ya madhumuni yaliyokusudiwa. Kwa kufanya hivyo taasisi hizo zitakuwa zinazingatia misingi ya kisheria ya faragha na heshima kwa haki za watu binafsi.

"Katika dunia ya sasa inayotawaliwa na teknolojia na matumizi makubwa ya taarifa za watu, ni muhimu kwa maafisa wa ulinzi wa taarifa binafsi kuelewa wajibu wao wa kisheria na kiutumishi. Misingi ya ukusanyaji wa idadi ya taarifa kulingana na makusudi husika , usalama wa taarifa, uhifadhi sahihi na usiri ni nguzo kuu katika kulinda haki ya faragha ya mtu binafsi,"alisema Bi. Hellen

Katika mafunzo hayo, washiriki walipata fursa ya kujadili mifano halisi ya changamoto wanazokutana nazo kazini na kushiriki katika mazoezi kwa vitendo yaliyowasaidia kuweka mikakati madhubuti ya kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi watakaporudi kwenye taasisi zao.

Mafunzo haya yanatarajiwa kuwa chachu ya maboresho katika usimamizi wa taarifa binafsi ndani ya taasisi mbalimbali, sambamba na utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini.



"Hata wale wanaosafirisha Taarifa Binafsi kwaajili ya kwenda kuzitunza mtandaoni **'Cloud Server'** wanapaswa kupewa kibali na PDPC



# Kusafirisha Taarifa Binafsi Nje ya Nchi ni lazima uwe na Kibali cha PDPC

Taarifa Binafsi yoyote inayoenda nje ya nchi ni lazima ipatiwe kibali na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC).

Haya yalisemwa Agosti 22,2025, Morogoro Mjini na Bw. Innocent Mungy, Mkuu wa Uhusiano na Mawasiliano - PDPC wakati akitoa mada ya namna ya kuomba kibali cha kusafirisha Taarifa Nje ya Nchi kwenye Mafunzo Maalumu ya Maafisa Ulinzi wa Taarifa (DPO),ambapo amesema hilo ni takwa la Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 . Hivyo taasisi, kampuni au mtu yoyote anaesafirisha Taarifa Binafsi nje ya mipaka ya Tanzania anapaswa kuomba kibali PDPC.

**"Hata wale wanaosafirisha Taarifa Binafsi kwaajili ya kwenda kuzitunza mtandaoni 'Cloud Server' wanapaswa kupewa kibali na PDPC na wakati wa kuomba kibali hicho wanatakiwa kusema hiyo 'server' ipo nchi gani, mtoa huduma ni nani na ni taarifa zipi wanazozisafirisha"** Alisema Bw.Mungy



# MAKALA MAALUMU

## Vyeti vya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) na Faida zake kwa Taasisi za Kibiashara Nchini.



Katika ulimwengu huu wa Mapinduzi ya Nne ya Viwanda unaoendeshwa kisasa kwa teknolojia na mifumo mbalimbali ya kidijitali, taarifa binafsi zimekuwa rasilimali muhimu kwa taasisi nyingi ikiwemo za kibiashara. Ninaposema taarifa binafsi namaanisha ni zile taarifa zinazoweza kumtambulisha mtu au utu wake, mfano **majina, anwani, namba za simu, taarifa za kifedha, taarifa za kiafya** n.k. Taarifa hizi zinatumika katika shughuli mbalimbali za biashara iwe uuzaji,ununuaji au kutoa huduma kwa wateja. Hata hivyo, matumizi yasiyo sahihi ya taarifa hizi yanaweza kusababisha athari kubwa kwa wateja na taasisi husika.

Hivyo ili kulinda haki za wananchi na kuhakikisha taasisi zinawajibika katika matumizi sahihi ya taarifa binafsi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Bunge lake tukufu ilitunga Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 (PDPA), na kuanzisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) kama chombo rasmi cha kusimamia utekelezaji wake.

Kupitia tume hii, taasisi zote zinazokusanya na kuchakata taarifa binafsi nchini zinapaswa kusajiliwa na kupata Vyeti husika kutoka PDPC, yaani kupata Cheti cha ukusanyaji wa taarifa binafsi na Cheti cha uchakataji wa taarifa binafsi, hatua ambayo inaleta manufaa mengi kwa taasisi ila kwaleo kupitia makala hii naomba nifahamishe walau kwa uchache faida nane (8) za taasisi za kibiashara kuwa na Vyeti kutoka PDPC:-

### 1. Kuongeza Uaminifu na Heshima ya Taasisi

Vyeti vya PDPC ni alama ya uadilifu na uwajibikaji. Wateja, washirika wako wa kibiashara na umma kwa ujumla wanapata imani zaidi wanapoona taasisi imesajiliwa rasmi na PDPC. Uaminifu huu ni nyenzo muhimu katika kujenga mahusiano endelevu ya kibiashara.

### 2. Uzingatiaji wa Sheria (Compliance)

Kusajiliwa chini ya PDPA kunahakikisha taasisi inafuata matakwa ya kisheria katika ukusanyaji, uhifadhi, matumizi na usambazaji wa taarifa binafsi. Hii inalinda taasisi dhidi ya adhabu, faini, au migogoro ya kisheria inayoweza kujitokeza kutokana na ukiukaji wa Sheria za ulinzi wa taarifa binafsi, Sura ya 44.

### 3. Kulinda Sifa na Kuepuka Madhara ya Kidijitali

Katika zama hizi za kidigitali, uvujaji wa taarifa au matumizi mabaya ya taarifa binafsi yanaweza kuharibu sifa ya biashara kwa muda mfupi. Vyeti vya PDPC ni kinga ya sifa ya taasisi kwa sababu vinahakikisha mifumo ya usalama wa taarifa imewekwa na inatekelezwa ipasavyo.

### 4. Kuongeza Ushindani wa Kibiashara
Taasisi zilizosajiliwa PDPC na kupata vyeti zinakuwa kwenye nafasi nzuri sokoni, kwakua wateja wa kisasa wanapendelea kufanya biashara na taasisi zinazoweka kipaumbele katika usalama wa taarifa zao. Sambamba na hilo Vyeti vya PDPC pia vinaweza kuwa kigezo muhimu katika zabuni, mikataba au miradi ya kimataifa.

### 5. Kuboresha Usimamizi wa Ndani wa Taarifa
Mchakato wa usajili na kupata vyeti husika vya PDPC unahusisha tathmini ya mifumo ya ndani ya usimamizi wa taarifa. Hii inasaidia taasisi kuboresha taratibu zake za ukusanyaji, uhifadhi na upatikanaji wa taarifa, hivyo kuongeza ufanisi wa utendaji wa ndani.

### 6. Kuepuka Migogoro na Malalamiko ya Wateja
Taasisi inayofuata kanuni za PDPA hupunguza kwa kiwango kikubwa malalamiko ya wateja yanayohusiana na matumizi mabaya ya taarifa zao binafsi. Hii inajenga uhusiano wa kuaminiana na wateja na kupunguza gharama za kushughulika na migogoro ya kisheria.

### 7. Kutoa Fursa za Ubia na Uwekezaji
Wawekezaji wa kimataifa na mashirika ya nje mara nyingi wanahitaji uthibitisho wa ulinzi wa taarifa kabla ya kushirikiana na taasisi yoyote. Vyeti vya PDPC vinatoa uhalali na uaminifu wa kisheria unaohitajika ili taasisi iweze kushirikiana kimataifa kwa urahisi zaidi.

### 8. Kuchangia Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Kidijitali
Kupitia usajili na utekelezaji wa PDPA taasisi zinachangia katika kujenga jamii ya kidijitali salama na yenye uwazi katika kufikia lengo la Serikali la kukuza uchumi wa kidijitali nchini.

Naam, nimefika tamati ya makala haya, naamini kwanamna moja au nyingine upata kujifunza mengi kuhusu umuhimu wa Vyeti vya PDPC kwa taasisi za kibiashara. Kikubwa naomba zingatia hili usajili wa taasisi ya kibiashara na kupata Vyeti husika kutoka PDPC si suala la hiari bali ni hatua ya kimkakati na kisheria, pia ni uwekezaji katika uadilifu, usalama na uendelevu wa biashara hivyo kama bado hujaisajili taasisi yako PDPC mpaka sasa basi naomba uisajili na kupata vyeti husika kwa maslai mapana ya Nchini na biashara yako.

Kumbuka kujisajili PDPC na kupata vyeti husika ni uamuzi sahihi kwa taasisi yoyote inayotaka kuendelea kuwa taasisi imara inayoaminika na yenye sifa ya ushindani katika soko la kidijitali.





**Wakili Humphrey Mtuy**, Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi **(PDPC)** akitoa wasilisho la Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Maadili ya Kidigitali na Faragha kwa wanachama wa TAWCA, Septemba 18, 2025 jijini Arusha.

# Elimu ya Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi yawafikia Wanawake Wahasibu Nchini

Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Wakili Humphrey Mtuy, Septemba 18,2025 alishiriki Mkutano wa nane (8) wa Uongozi wa Wanawake - 2025 ulioandaliwa na Chama cha Wahasibu wanawake Tanzania (TAWCA) na kufanyika jijini Arusha.

Katika Mkutano huo Wakili Mtuy amepata fursa ya kutoa wasilisho la Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Maadili ya Kidigitali na Faragha ambapo ametoa wito kwa wanawake wahasibu na wakaguzi wa ndani wa hesabu za fedha kuhakikisha wanalinda faragha za wateja na watumishi wa Taasisi zao kwa kutunza vema taarifa binafsi wanazozikusanya na kuchakata wakati wa kutoa huduma.

“Aina ya taarifa binafsi mnazozifanyia kazi kila siku zipo kwenye kundi la taarifa binafsi nyeti ambazo zisipotunzwa kwa uangalifu zinaweza kuleta madhara kwa mtu binafsi ama kwa taasisi, hivyo natoa wito kwenu kuhakikisha mnafanya uzingatiaji wa matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 ili kuepuka matatizo yote yanayoweza kutokana na uvunjifu wa Sheria hii” alisema Wakili Mtuy.

Aidha Wakili Mtuy ametumia jukwaa hilo kuweka bayana adhabu zinazoweza kutolewa na PDPC endapo mkusanyaji na mchakataji wa taarifa binafsi asipotimiza matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44.

“Kwa mujibu wa Sheria endapo Mkusanyaji na Mchakati wa taarifa asipozingatia Sheria hii ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 wakati wa utekelezaji wake wa majukumu anaweza kupewa adhabu mbalimbali ikiwemo faini, vifungo au vyote kwa pamoja” Alimalizia Wakili Mtuy.

PDPC imeshirikiana na Chama cha Wahasibu Wanawake Tanzania (TAWCA) kudhamini Mkutano huu uliodhuriwa na wanawake zaidi ya 300 kutoka sekta mbalimbali nchini ikiwemo wahasibu na wakaguzi wa ndani.



Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi **(PDPC)** , **Wakili Humphrey Mtuy**, akitoa wasilisho kwenye Mkutano wa Nane (8) wa Uongozi wa Wanawake - 2025.



# HABARI PICHA



Kutoka Kushoto ni CPA. Amina Ramadhani Haighai, Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu - PDPC, akiwa na CPA. Theresia Mihayo, Mkaguzi Mkuu wa Ndani - PDPC kwenye Mkutano wa nane wa Uongozi wa Wanawake 2025, uliofanyika Septemba17 - 19, 2025 Jijini Arusha. Mkutano huu uliandaliwa na Chama cha Wahasibu Wanawake Tanzania (TAWCA) na ulibebwa na kauli mbiu ya Muongo wa Ubora: Kuwawezesha Viongozi, Kuendesha Mabadiliko.

CPA. Apaisaria Ulomi, Mkaguzi wa Ndani, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), akifatilia kwa makini Mada ya Maadili na Saikolojia Kazini iyotolewa na Dkt. Chris Mauki - Mtaalamu wa Saikolojia kutoka Chuo Kikuu Dar es salaam (UDSM) wakati wa Mkutano wa nane wa Uongozi wa Wanawake - 2025.

CPA. Apaisaria, ni miongoni mwa watumishi wa PDPC walioshiriki kongamano hili la siku tatu (3) lililoandaliwa na Chama cha Wahasibu Wanawake Tanzania (TAWCA) na kufanyika Jijini Arusha kuanzia Sptemba 17 - 19, 2025.






Afisa Habari wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Bi. Evelyne Francis akitoa elimu ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa baadhi ya washiriki wa Mkutano wa nane (8) wa Uongozi wa Wanawake 2025, ulioandaliwa na Chama cha Wahasibu Wanawake Tanzania (TAWCA) na kufanyika jijini Arusha mwezi Septemba, 2025.



Ni baadhi ya Watumishi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) walioshiriki Mkutano wa nane (8) wa Uongozi wa Wanawake - 2025, ulioandaliwa na Chama cha Wahasibu Wanawake Tanzania (TAWCA) na kufanyika jijini Arusha mwezi Septemba, 2025. CPA. Amina Ramadhani Haighai,( wa kushoto) Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu - PDPC na CPA. Apaisaria Ulomi, (wa kulia) Mkaguzi wa Ndani - PDPC.



**JARIDA HILI LIMETOLEWA NA:**

TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI (PDPC),
S. L. P 1105,
1 Mtaa wa Moshi, Viwandani,
41102 DODOMA.